

**UGATUZI**

Kiwanda cha Sh800 milioni cha kubadilisha maji taka kujengwa

Uk 6



**TEKINOLOJIA**

Kaunti kuwekeza katika tekinolojia ya kubadilisha taka kuwa mbolea.

UK 3

**UVUMBUZI**

Egerton yaunda aina mpya ya mbegu za mimea za kuhimili mabadiliko ya tabianchi



UK 9

www.mygov.go.ke

JANUARI 17, 2023

# MyGov.

TATHMINI YAKO YA WIKI

TOLEO No. 27/2022-2023

# Furaha KTDA ikilipa wakulima wa chai bonasi ya Sh5.5b

Waziri wa Kilimo Mithika Linturi alisema kwamba mnamo Desemba 2022 katika Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka wa KTDA (AGM), aliomba Bodi kufikiria kulipa bonasi ndogo kwa wakulima Januari ili waweze kulipa karo ya shule ikizingatiwa shule zitafunguliwa baadaye mwezi huu



**Waziri wa Kilimo (CS) Mithika Linturi akihutubu jijini Nairobi alipotangaza bonasi ya Sh5.5B ambayo KTDA italipa wazalishaji majani chai wadogo.**

**NA JOSEPH NG'ANG'A (KNA)**

Shirika la Ustawi wa Chai Kenya (KTDA) limetoa bonasi ndogo ya Sh.5.5 bilioni kwa wakulima wa mashamba madogo ya chai nchini kuwakinga dhidi ya kupanda kwa gharama ya maisha. Waziri wa Kilimo Mithika Linturi alisema kwamba mnamo Desemba 2022 katika Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka wa KTDA (AGM), aliomba Bodi kuwazia kulipa bonasi ndogo kwa wakulima Januari ili waweze kulipa karo ya shule ikizingatiwa shule zitafunguliwa baadaye mwezi huu. Linturi alisema kwamba KTDA inasimamia jumula ya viwanda 71 na serikali imejitolea kusaidia kuimarisha mapato ya wakulima wa chai.

"Sekta ya Chai ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wetu kwa kuwa inachangia asilimia mbili ya pato la nchi (GDP) na asilimia nne ya pato la kilimo, huku sekta hiyo ikisaidia 650,000 anbao viwanda vyao vinasimamiwa na KTDA," alisema.

Linturi alieleza kuwa kutokana na habari ambazo wamekuwa wakipata, uzalishaji wa chai umeongezeka katika miezi ya Novemba na Desemba kutokana na mpango wa ruzuku ya mbolea ambao serikali inatekeleza.

"Kama serikali, tutaendelea kufanya kazi kuhakikisha kwamba gharama

ENDELEA UK 2



**Takwimu za wiki**

**82M**
Kiasi cha pesa kilichotumika kwenye mpango wa kitaifa chini ya Wizara ya Kilimo kupiga jeki wakulima Bungoma

**200**
Idadi ya malori ambayo hutupa taka katika jaa la taka la Gioto katika mtaa wa London, Nakuru kila siku

**14,000**
Familia katika kaunti tano ambazo zilinufaika kutokana na chakula cha msaada chini ya mpango wa Wakenya Tulindane

**100M**
Lita za mafuta ambazo Kenya Pipeline itahifadhi baada ya kununua mabomba mapya

**25,000**
Idadi ya vituo vya Wifi kote nchini ambavyo serikali inanuia kuanzisha

**30**
Maharagwe kwenye kila ganda ambazo aina za kisasa za mbegu huzalisha



## Kenya Pipeline yaimarisha uwezo wake, kuhifadhi mafuta zaidi

**NA MUTISO MBITHI (MYGOV)**

Kampuni ya Kenya Pipeline, imekamilisha mchakato wa kutwaa kampuni ya kusafisha mafuta inayomilikiwa na serikali ya Kenya Petroleum Refineries Ltd (KPRL) iliyoko Changamwe, Mombasa kuhifadhi bidhaa zaidi za mafuta baada ya kampuni hiyo kusitishwa shughuli zake. Kampuni ya Kenya Petroleum Refineries ilikuwa ya pekee ya kusafisha mafuta Afrika Mashariki kutoka Mombasa lakini tangu ilipoimamisha shughuli zake miaka iliyopita, mashine zake zilipitwa na wakati kutokana na kuibuka kwa tekinolojia mpya, na matangi yake makubwa eneo la Kipevu hayatumiki.

Baada ya kutwaa matangi ya KPRL, KPC itaanza mchakato wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi mafuta kwa kuongeza lita zaidi ya 100 milioni za bidhaa za mafuta ya kusafirisha kwa wauzaji wa mafuta ndani ya nchi. Afisa wa cheo cha juu wa Kampuni ya Kenya Pipeline aliyezungumza na MyGov katika matangi ya kuhifadhi mafuta ya Kipevu, Mombasa alisema kwamba kutwaa matangi hayo kutakuwa kwa mpango wa kukodisha. KPRL ilianzishwa 1960 na serikali ya Kenya na kampuni ya Shell and British Petroleum na iliinuiwa kuhudumia eneo la Afrika Mashariki kwa kusafisha mafuta yaliyoagizwa bila kusafishwa na kuuza bidhaa za mafuta yaliyosafishwa kwa masoko ya Afrika Mashariki.

KOMESHA COVID-19
" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"
HOMA
KIKOHOZI
KUSHINDWA KUPUMUA
MAUMIVU KOONI
KUUMWA NA KICHWA

# Furaha KTDA ikilipa wakulima wa chai bonasi ya Sh.5.5 Bilioni

ENDELEA KUTOKA UK 1

ya uzalishaji utapungua ili wakulima wetu wanufaike," alisema Waziri huyo na kuongeza kuwa kama wizara, wameagizwa na Rais kuhakikisha wakulima wa chai wananufaika na zao lao.

Alisema kwamba serikali inatafuta pesa za kufadhili ujenzi wa mitambo 11 ambayo itakuwa ikitengeneza chai ambayo inanunuliwa kwa bei nzuri katika soko ulimwenguni. Hatua hii itahakikisha kwamba Wakulima wa Kenya wataweza kupata pesa zaidi kutoka kwa zao lao.

"Pia serikali inaahidi kwamba ndani ya mwaka huu itaongeza uongezaji wa thamani katika chai yetu ili tuweze kupata angalau asilimia 50 ambayo itasaidia kupunguza kiwango

> Niunda kikosi cha kuharakisha utaratibu wa kulainisha ugavi wa mapato- Mvurya



cha chai isiyotengenezwa tunayouza nje ya nchi," alisema Linturi. Alisema kwamba wa Wizara imealika wadau wa sekta ya kibinafsi kuwekeza katika uongezaji thamani, huku serikali ikijiandaa kujenga vituo vya watumiaji katika maeneo spesheli ya uchumi hasa katika Dongo Kundu, ambako uongezaji thamani chai utakuwa ukifanyiwa.

"Vituo hivi vya watumiaji vitakapokamilika, wale ambao hawatakuwa na uwezo wa kujenga mitambo ya kuongeza thamani wataweza kupata vituo vya serikali na kupakia chai yao na kuiuza nje ya nchi," alieleza Waziri.

Linturi aliongeza kuwa balozi za Kenya ni mabalozi wa chai ya Kenya na wanajaribu kuzihimiza ziendelee kutafuta masoko ya chai ya Kenya na mazao mengine. "Masoko yetu makubwa ya chai ni Pakistan na Egypt na bado tunahisi kwamba tunaweza kupata zaidi kwa kutafuta masoko mengine," alisema. Mwenyekiti wa KTDA Holdings David Ichoho alisema kwamba Sh2.7 bilioni kati ya zilizotolewa ni malipo ya bonasi ndogo ya viwanda, ambazo wakurugenzi walipitisha maazimio ya kulipa wakulima wao bonasi ndogo.

Ichoho alisema kwamba Sh.2.8 bilioni zinazosalia zitalipwa wakulima kwa chai waliyopeleka viwandani mwezi Desemba.

# Gov't invites international actor to film next movie project on Kenyan grounds

BY MOSES WEKESA (KNA)

Kenya has invited an international movie superstar, Leonardo DiCaprio, to film his next movie project in the country to educate, motivate and encourage local film industries and as part of efforts to promote local tourist attraction sites to an international audience.

Youth Affairs, Sports and Arts Cabinet Secretary, Ababu Namwamba, announced that Kakamega Forest, Kisumu and Homa Bay are some of the sites selected, where scenes for the movie will be filmed.

"Leonardo DiCaprio is coming to Kenya to shoot a big movie. We have selected places which we also want to see grow as tourist destinations," he noted. Namwamba further said the engagement with the film actor is part of the government's efforts to improve the creative sector in general which includes film, music, sports, talents among others.

Speaking in Kakamega, CS Namwamba said the National Government will work with the Kakamega County Government to develop sports and the creative sector in general.

"We have agreed with Governor Ferdinand Barasa to complete the ongoing works of Phase II of upgrading Bukhungu Stadium. On completion of terraces the stadium will have a sitting capacity of 30, 000 spectators," he noted.

Once Phase II is completed, the CS announced that the National Government will take over to complete Phase three, which will include upgrading of facilities, ablution blocks, hospitality facilities and world standard changing rooms.

"And since Kenya is bidding to host the 2027 African Cup of Nations, I see games of Afcon being played at Bukhungu Stadium. We will also ensure when we have big events the Stadium will host," he noted.

REPUBLIC OF KENYA

PRIVATIZATION COMMISSION
Enhancing Kenya's Productive Capacity

## MWALIKO WA TENDA

### TENDA YA KUTOA BIMA YA GPA KWA WAFANYAKAZI NA BODI, BIMA YA WIBA NA BIMA YA MAISHA KWA WAFANYAKAZI (KANDARASI) NA RFP KWA UTOAJI WA HUDUMA ZA USHAURI KUHUSU UBINAFSISHAJI WA AGRO CHEMICAL AND FOOD COMPANY LIMITED (ACFC)

Privatization Commission (PC) inaalika maombi ya tenda kutoka kwa wanaotoa huduma za bima na washauri kuhusu uuzaji kutoka huduma zifuatazo na ushauri kama inavyofafanuliwa kwenye stakabadhi tofauti za tenda/RFP.

| JINA LA TENDA | NAMBARI YA TENDA | SIKU NA WAKATI WA KUFUNGWA | WALIOTENGEWA |
|---|---|---|---|
| 1) Tenda ya utoaji wa bima ya GPA kwa wafanyakazi na Bodi, Bima ya Wiba na ile ya Maisha kwa wafanyakazi (Kandarasi) – (Marudio ya tangazo)<br>**Tarehe ya uzinduzi – 17.01.2023** | PC/08/2022 – 2023 | 31.01.2023 saa 5.00 asubuhi | Wazi kwa watoaji huduma za bima ***(wazi kwa mashirika ya bima yaliyosajiliwa na kampuni za mawakala wa bima)*** |
| 2) RFP ya utoaji wa Huduma za Ushauri kuhusu ubinafsishaji wa Agro Chemical and Food Company Limited (ACFC)<br>**Tarehe ya uzinduzi – 17.01.2023** | PC/09/2022 – 2023 | 31.01.2023 saa 5.00 asubuhi | Wazi kwa Wataalamu waliohitimu |

Wanaopenda kutuma maombi wanaweza kuchukua nakala ya stakabadhi za tenda bila malipo, kutoka kwa tovuti ya Tume www.pc.go.ke au https://www.tenders.go.ke/website na wanapasa kufahamisha Tume mara moja kupitia kwa email info@pc.go.ke.

**MKURUGENZI MKUU/CEO**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

## KENYA ORDNANCE FACTORIES CORPORATION

KOFC
KENYA ORDNANCE FACTORIES CORPORATION

## NOTISI YA TENDA

Kenya Ordnance Factories Corporation (KOFC) inaalika maombi kutoka kwa wauzaji kutoa huduma zifuatazo:

| Nambari ya Tenda | Maelezo ya Huduma | Tarehe ya mwisho |
|---|---|---|
| KOFC/OT/GEN/001/22-23 | Utoaji wa Huduma za Bima | 4:00 asubuhi 01 Februari 2023 |
| KOFC/OT/BAKERY/002/22-23 | Kununua na kusambaza sukari | 4:00 asubuhi 02 Februari 2023 |
| KOFC/OT/ BAKERY /003/22-23 | Kununua mchanganyiko wa vifaa vya kupakizia | 4:00 asubuhi 02 Februari 2023 |
| KOFC/OT/GEN/002/22-23 | Utoaji wa huduma za uchukuzi | 4:00 asubuhi 02 Februari 2023 |

Wauzaji bidhaa wanaweza kuchukua stakabadhi za tenda bila malipo kutoka kwa tovuti yetu **www.kofc.co.ke**. Stakabadhi zilizopakuliwa zinapasa kujazwa kwa mujibu wa maagizo yaliyotolewa na kuwekwa ndani ya sanduku la tenda katika Kenya Ordnance Factories Corporation (Lango Kuu) kwenye barabara ya Eldoret - Kitale mnamo au kabla ya tarehe zilizoonyeshwa dhidi ya kila tenda saa 4.00 asubuhi.

Hati zilizopangwa kulingana na kurasa; Moja asili na Nakala yake zilizowekwa ndani ya bahasha iliyojazwa Nambari ya Tenda na Maelezo pamoja na Dhamana ya Tenda ya kiasi kilichoonyeshwa kwenye kila stakabadhi za tenda kutoka kwa taasisi ya kifedha iliyoidhinishwa na Benki Kuu ya Kenya inapasa kutumwa kwa:

**Kenya Ordnance Factories Corporation**
**P.O Box 6634-30100**
**Eldoret-Kitale Road**
**Kenya**
**Tel: +254 794 517 532**

Tenda zitafunguliwa mara moja mbele ya waliotuma maombi au wawakilishi wao ambao wataamua kuhudhuria.

Wanaotuma maombi wanahimizwa kutembelea mara kwa mara tovuti ya KOFC kupokea maelezo zaidi/stakabadhi za ziada kuhusu tenda.
Wanaotuma maombi wanashauriwa kukagua sampuli za vifaa vya kupakizia kabla ya kuwasilisha maombi ya tenda. Sampuli zinapatikana katika lango kuu la kuingia katika KOFC nyakati za kazi.

Maombi ya tenda yatakayowasilishwa kuchelewa hayakubaliwa
**M K ONG'OYI**
**Meja Jenerali**
**Mkurugenzi Mkuu**

KENYA VISION 2030






# Kaunti kuwekeza katika tekinolojia ya kubadilisha taka kuwa mbolea

**NA JANE NGUGI (KNA)**

Serikali ya kaunti ya Nakuru inashirikiana na sekta ya kibinafsi ili kuinua uwekezaji katika tekinolojia za kubadilisha taka kuwa mbolea, kawi na mafuta.

Afisa Mkuu wa Mazingira, Kawi, Mali Asili na Mabadiliko ya Tabia nchi katika kaunti hiyo Bw Kennedy Barasa alisema kwamba uzalishaji wa stima kutoka taka una uwezo wa kupunguza uharibifu wa mazingira na kuongeza nafasi za ajira. Akizungumza alipoongoza timu kutoka Bodi ya Usimamizi wa Jiji katika ziara ya jaa la Gioto mtaani London, Barasa alisema kwamba ukuaji haraka wa miji, kuimarika kwa hali ya uchumi ya na viwanda kumebadilisha usimamizi wa taka kuwa moja wapo ya changamoto kuu zinazokumba miji mikuu Kenya. “ Hii inahitaji Kaunti ya Nakuru kupunguza, kutumia tena, na kubadilisha taka. Mipango mizuri ya usafi inaweza kusaidia kaunti yetu kuimarisha hali ya sasa ya ushughulikiaji wa taka na kuokoa pesa. Ni lazima tutumia kwa dharura uwezo wa kawi tulio nao katika taka kupitia tekinolojia zinazopatikana za kufanya taka kuwa kawi na pia kuweka mipango ya mikakati ya utekelezaji wa tekinolojia hizi,” alisema Afisa Mkuu huyo. Wawekezaji kadhaa, wa humu nchini na kimataifa, wamewahi kuomba serikali ya kaunti kubadilisha taka kuwa biashara lakini hatimaye wananyamaza.

> Tunahitaji teknolojia ya kisasa kusaidia namna tunashughulikia takataka," -Barasa

Serikali ya kaunti tayari imeanza kukarabati jaa hilo la ekari 30 na imechukua hatua za kuzuia uvujaji wa taka katika barabara ya Nakuru kwenda Kabarak msimu wa mvua. Idara ya mazingira pia imegawanya jaa hilo katika sehemu ambazo taka inayoweza kubadilishwa na inayooza zinatupwa kwa kutenganishwa. Barasa, ambaye aliandamana na Meneja wa Bodi ya Jiji la Nakuru Bw Gitau Thabanja na Afisa Mkuu wa Mipango ya miji Bw Kamau Kuria alisema kwamba kaunti inazungumza na wadau tofauti kuhusu usimamizi na njia bora za kubadilisha na kukarabati jaa hilo. Alisisitiza umuhimu wa kuzingatia uwezo wa kubadilisha taka kuwa kawi ili kuleta mabadiliko chanya kwa jamii.



Afisa Mkuu huyo alisema, “ Tunahitaji tekinolojia bunifu na mbinu ambazo zitaleta mabadiliko kuhusu tunavyofikiria, kutumia na kufanya na taka za nyumbani, viwandani na biashara. Nakuru inafaa kuzingatia mambo matano ya kufikiria, kukataa, kupunguza, kutumia upya na kubadilisha ili kugeuza taka kuwa mali.”

Ukosefu wa usimamizi unaofaa wa taka umesababisha uchafuzi wa hewa, mchanga na maji, kutishia afya ya umma, mazingira na viumbe na kuongezeka kwa viwango vya taka katika maziwa na mito ya Nakuru.

Barasa aliongeza kuwa kutoka ubunifu katika usimamizi wa taka kupitia mbinu tano, Nakuru inaweza kutatua changamoto hiyo na pia kuunda ajira, kuinua ukuaji wa uchumi, kuimarisha afya na mazingira. Alisema hii inachangia kuwa na kaunti ya watu wenye furaha, salama na afya nzuri na kuokoa pesa nyingi za kaunti.

# Serikali kuchunguza viwanja vipya vilivyojengwa kote nchini-Waziri

**NA JUSTUS ANZAYA (KNA)**

Waziri wa Michezo, Utamaduni na Sanaa Ababu Namwamba ameagiza uchunguzi wa viwanja vyote vilivyojengwa majuzi kote nchini kubaini iwapo pesa zilizowekezwa katika vituo hivyo vya Michezo zilitumiwa vyema. Namwamba aliyezungumza baada ya kutembelea Uwanja wa maonyesho ya Kilimo wa Njukiri kaunti ya Embu alifichua kwamba serikali inapanga kujenga uwanja wa kisasa katika eneo hilo kwa maandalizi ya sherehe za Madaraka Dei Juni 1, 2023. Waziri alisema kwamba uwanja huo utakapokamilika utakuwa na vifaa vya kisasa vya michezo. “ Nina matumaini kwamba tutajenga uwanja wa kisasa hapa ukiwa na vifaa vingi vya michezo,” alisema.



**Waziri wa Michezo, Utamaduni na Sanaa Ababu Namwamba**

Baada ya kutembelea uwanja wa Moi uliojengwa majuzi

Embu wakati wa utawala ulioondoka, Waziri alisikitika kwamba mwanakandarasi alifanya kazi mbaya na kwamba uwanja huo hauakisi kiwango cha pesa ambacho serikali ilitenga kwa ujenzi wa uwanja huo.

Alilalamikia hali mbaya ya uwanja wa michezo wa Moi ambao unasemekana uligharimu Sh180 milioni, akisema hakuna kilichofanywa kamwe katika uwanja huo.

“Ni aibu kubwa kwa mtu kudai alitumia Sh180 milioni kufanya kazi mbaya tunayoona hapa,” alisema na akaongeza kuwa ameandikia barua Mhasibu Mkuu afanye uchunguzi wa viwanja vyote vipya vilivyojengwa nchini miaka ya hivi majuzi kote nchini.

Namwamba alisema kwamba ukaguzi huo utakapokamilika, hatua za kisheria zitachukuliwa yeyote atakayepatikana alihusika na ubadhirifu wa pesa zilizonuiwa ujenzi wa viwanja

Alisema kwamba amepatia Mkaguzi Mkuu siku 60 kufanya uchunguzi wa viwanja vya michezo vilivyojengwa majuzi kote nchini.

Akishukuru serikali kwa kupanga kujenga uwanja wa michezo katika uwanja wa maonyesho ya kilimo, Gavana Cecily Mbarire alisema kwamba kaunti ya Embu itanufaika pakubwa kutoka ujenzi wa uwanja huo wa michezo.

“ Ninafuraha kwamba serikali iliona inafaa kujenga uwanja wa michezo na tuko na furaha kwa sababu tunajua mazuri utakaoleta,” alisema Mbarire.

Kuboreshwa kwa uwanja wa michezo wa Moi na ujenzi wa uwanja katika uwanja wa maonyesho ya kkilim Njukiri umepangwa kuanza Februari mwaka huu.

REPUBLIC OF KENYA

PSASB
PUBLIC SECTOR ACCOUNTING STANDARDS BOARD (KENYA)

## BODI YAVIWANGO VYA UHASIBU SEKTA YA UMMA

## NAFASI ZA KAZI

Bodi ya Viwango vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (PSASB) ni Idara Huru ya Serikali inayojitegemea iliyoanzishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFM) Na.18 ya mwaka 2012. Bodi ina jukumu la kutoa mifumo na kuweka viwango vya uendelezaji na usimamizi wa uhasibu, mifumo ya ukaguzi wa fedha za na wa ndani kwa vyombo vyote vya serikali na mashirika ya umma.

Ili kuongeza uwezo wa kitaasisi kutekeleza majukumu yake, Bodi inatafuta kuajiri watu waliohitimu na wenye uwezo kujaza nafasi zifuatazo zilizoachwa wazi:

| S/No. | Namba | Nafasi | Kiwango | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | PSASB/1/2023 | Meneja Fedha na Hesabu | ASB 3 | 1 |

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Maelezo ya kina ya kazi na mahitaji ya nafasi hiyo hapo juu yanapatikana katika **www.psasb.go.ke/careers**

Iwapo unaweza kuonyesha kwa uwazi uwezo wako wa kutimiza mahitaji yaliyowekwa, tafadhali tuma ombi lako kupitia kiungo kilichotolewa kwenye tovuti ya PSASB na utume CV yako kupitia barua pepe, nakala za vyeti vya elimu na kitaaluma na hati nyingine yoyote muhimu kwa anwani **recruitment@psasb.go.ke.**

Tafadhali onyesha nambari ya marejeleo juu ya mada ya barua pepe. Wagombea walioorodheshwa watahitajika kuwasilisha vyeti vyao vya kibali/kutii kutoka kwa CID, HELB, EACC, CRB & KRA. Maombi yote yanapaswa kupokelewa kabla ya tarehe **2 Februari, 2023** saa **5.00 jioni.**

***PSAB ni mwajiri anayetoa nafasi sawa za ajira. Ombi la yeyote atakayepatikana akidanganya litafutiliwa mbali. PSAB huwa haitozi malipo yoyote kutuma maombi ya kazi. Wanawake, Vijana na Walemavu wanahimizwa kutuma maombi.***

Promoting Sound Financial Reporting and Internal Audit Standards in the Public Sector

CPA Centre, 8th Floor, Thika Road, Ruaraka. P.O Box 38831 - 00100, Nairobi, Kenya. Tel: 020 251 1557
www.psasb.go.ke. email: info@psasb.go.ke

**" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"**




REPUBLIC OF KENYA

COMPETITION AUTHORITY OF KENYA
*Creating efficient markets for consumers*

## TANGAZO LA ZABUNI

Mamlaka ya Ushindani Kenya (Mamlaka) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Ushindani Namba.12 ya 2010. Jukumu la Mamlaka ni kuimarisha ustawi wa watu wa Kenya kwa kukuza na kulinda ushindani wenye ufanisi katika masoko na kuzuia ukosefu wa haki na mwelekeo potoshi.

Mamlaka inakaribisha zabuni kutoka kwa mashirika yenye nia na yenye uwezo kutoa zabuni zifuatazo:

| No | Namba ya Marejeleo | Maelezo ya Tenda | Uhitimu | Tarehe ya kufunga na wakati |
|---|---|---|---|---|
| 1. | CAK/TEND/003/2022-2023 | Utoaji wa Usaidizi wa Mfumo na Utunzaji wa Mfumo wa Kusimamia Kesi (CMS) na Mfumo wa Kudhibiti Hati (DMS). | Wazi kwa Wote | 31 Januari 2023, saa 12.00 Mchana |
| 2. | CAK/DISP/01/2022-2023 | Utupaji wa Magari Yasiyotumika | Wazi kwa Wote | 31 Januari 2023, saa 12.00 Mchana |

Nyaraka za zabuni zinapatikana kutoka kwa Tovuti ya Taarifa ya Ununuzi wa Umma (PPIP) **https://www.tenders.go.ke** na Tovuti ya Mamlaka **www.cak.go.ke**. Zaidi ya hayo, makampuni ya zabuni yanapaswa kuwasilisha taarifa/mawasiliano yao kwa Meneja wa Mamlaka, Usimamizi wa Mfumo wa Usambazaji kupitia barua pepe: **scm@cak.go.ke** kabla ya tarehe ya mwisho ya uhifadhi wa kumbukumbu na mawasiliano ya siku zijazo, ikiwa ni pamoja na ufafanuzi na/au nyongeza, iwapo kuna yoyote

Nyaraka za zabuni zilizokamilishwa ipasavyo ziwasilishwe katika bahasha iliyofungwa, iliyo na alama ya jina la zabuni na nambari ya kumbukumbu. Hati ziwekwe kwenye sanduku la zabuni lililoko kwenye Orofa ya chini ya Makao Makuu ya Mamlaka au zitumwe kwa anwani iliyo hapa chini.

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Ushindani ya Kenya,**
**Shirika la Reli la Kenya, Makao Makuu, Orofa ya Chini,**
**P.O.Box 36265-00200,**
**Barabara ya Haile Selassie, Workshop Road,**
**NAIROBI.**

Zabuni zitafunguliwa baadaye katika Ukumbi wa Mikutano wa Mamlaka, Orofa ya Chini mbele ya wazabuni au wawakilishi wao wanaochagua kuhudhuria. Zabuni zilizochelewa hazitazingatiwa.

REPUBLIC OF KENYA

ICIFA
INSTITUTE OF CERTIFIED INVESTMENT AND FINANCIAL ANALYSTS

### SHERIA YA UWEKEZAJI NA WACHAMBUZI WA FEDHA, NA. 13 YA 2015

## TAARIFA YA VIGEZO VILIVYOIDHINISHWA VYA USAJILI

Sheria ya Wachambuzi wa Uwekezaji na Fedha, namba 13 ya mwaka 2015 (Sheria) inatoa nafasi ya uanzishwaji, mamlaka na kazi za Taasisi ya Wachambuzi wa Uwekezaji na Fedha (Taasisi), uchunguzi na usajili wa Wachambuzi Walioidhinishwa wa Uwekezaji na Fedha, na kwa madhumuni yaliyounganishwa.

Kwa mujibu wa vifungu vya 16 (2) na (3) vya Sheria ya Uwekezaji na Wachambuzi wa Fedha Namba 13 ya 2015 (IFA Act), Baraza la Taasisi ya Wachambuzi Walioidhinishwa wa Uwekezaji na Fedha, kwa kushauriana na Baraza la Mitihani, linatathmini kusajili kama Wanachama Kamili, watu ambao kwa sasa ni watendaji katika masuala ya fedha tasnia ya huduma na wana uzoefu wa angalau miaka kumi (10) kufikia tarehe 7 Juni 2017 ilimradi watu hao watimize vigezo vifuatavyo:

1. **kwamba wana ujuzi wa kutosha wa sheria za Kenya, ikiwa ni pamoja na sheria ya ushuru na sheria zinazosimamia masoko ya fedha kama ilivyobainishwa na Baraza la Mitihani (kasneb);**
2. **kwamba wana uzoefu wa kutosha katika uwekezaji na uchambuzi wa kifedha katika usimamizi mkuu kwa sasa;**
3. **kwamba wana mwenendo wa kitaaluma unaokubalika na tabia ya jumla ambayo kwa maoni ya Kamati ya Usajili inawafanya watu hao kuwa watu wanaofaa na wanaofaa kusajiliwa;**
4. **kwamba wawe na digrii husika, ikiwezekana Shahada ya Uzamili katika Fedha, Uwekezaji, Benki, Uchumi, Takwimu, Sayansi ya Hakimiliki, au shahada sawa na hiyo kutoka vyuo vikuu vinavyotambuliwa na kuthibitishwa;**
5. **kwamba wana sifa zinazofaa za kitaaluma, ikiwezekana CIIA, CFA, FIA, CPA, au sifa zinazolingana na CIFA, zinazotambuliwa na Taasisi; na**
6. **kwamba wanakidhi matakwa ya Sura ya 6 ya Katiba ya Kenya.**
   Waombaji watahitajika kufanya mtihani maalum utakaopelekea tathmini kufanywa kwa pamoja na Taasisi na Baraza la Mitihani, na pia watafanya mtihani wa maadili na uadilifu wa Taasisi kwa kuzingatia kifungu kidogo cha 8 (f) cha Sheria ya IFA. Kwa mujibu wa Sheria ya IFA, waombaji wanatakiwa kuridhisha Kamati ya Usajili kwamba wana mahitaji muhimu na wanastahili kusajiliwa kama wanachama Kamili wa Taasisi.

   Watu ambao wanastahiki kusajiliwa kama ilivyoainishwa katika mahitaji hapo juu wanaweza kuwasilisha fomu ya maombi iliyojazwa ipasavyo iliyojazwa kwa madhumuni haya pamoja na CV ya kina iliyosasishwa kupitia tovuti ya usajili ya mtandaoni ya Taasisi kwenye **www.icifa.co.ke** kuanzia tarehe **1 Januari 2023** hadi tarehe **31 Machi 2023.** Maombi yatakayotumwa baada ya tarehe ya mwisho hayatazingatiwa.

**2 Tarehe 8 Desemba 2022**

| | | |
|---|---|---|
| **FA Diana Muriuki-Maina** | **FFA Dr. Jonah Aiyabei** | **FA Einstein Kihanda** |
| **CEO/Katibu** | **Mwenyekiti, Kamati ya Usajili** | **Mwenyekiti wa Taasisi** |

REPUBLIC OF KENYA

KENYA POWER PENSION FUND

## NOTISI YA TENDA

Kenya Power Pension Fund inaalika mashirika kutoa huduma zifuatazo;

| NO. | JINA LA TENDA | NAMBARI YA TENDA | WALIO-HITIMU | TAREHE YA MWISHO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | UTOAJI WA HUDUMA ZA UTOA-JI CHETI CHA ISO 9001:2015 | KPPF/PROC/2-A/01/2023 | WAZI | Alhamisi Februari 2, 2023 saa 5.30 asubuhi |
| 2. | PROVISION OF INTERNAL AUDIT SERVICES | KPPF/PROC/2-A/02/2023 | WAZI | Jumanne Februari 7, 2023 saa 5.30 asubuhi |

Stakabadhi za tenda zinazofafanua mahitaji ya tenda zilizotajwa hapo juu zinaweza kupatikana kutoka kwa mtandao wa Kenya Power Pension Fund **www.kppf.co.ke** kuanzia **Januari 17, 2023** **bila malipo**. Wanaotuma maombi wanahitajika kutuma baruapepe kwa **tenders@kppf.co.ke ili kupokea ufafanuzi na/au mawasiliano inapohitajika.**

Stakabadhi za tenda zilizojazwa na kufungwa kwenye bahasha na kuandikwa **jina** na **nambari ya tenda** zinapasa kutumwa kwa: -

**CEO & TRUST SECRETARY**
**Kenya Power Pension Fund,**
**Stima Plaza Annex, Kolobot Road, Parklands**
**P.O Box 1548 – 00600 Nairobi, Kenya.**
**na kuwekwa ndani ya sanduku la tenda lililoko Ground floor, Stima Plaza Annex karibu na eneo la lifti.**

Ili kupokelewa mnamo au kabla ya tareje ya mwisho iliyoonyeshwa hapo juu. Tenda zitafunguliwa hapo baadaye mbele ya waliotuma maombi au wawakilishi wao ambao wataamua kuhudhuria katika Kenya Power Pension Fund, Stima Plaza Annex Ground floor, Kolobot Road, Parklands, Nairobi.

Isipokuwa kujibu ufafanuzi kutoka kwa KPPF, waliotuma maombi hawapaswi kuwasiliana au kujadili kuhusu swala lolote linalohusiana na tenda baada ya tarehe ya mwisho ya kutuma maombi na kabla ya kupokea ilani ya kupewa tenda au kutoshinda, inavyohitajika. Mawasiliano kama hayo yatafanya ombi kutupiliwa mbali.

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

Kenya Power

## MWALIKO WA ZABUNI

Kenya Power inaalika zabuni kutoka kwa wazabuni ili kutoa huduma zifuatazo:-

| NA. | NA. YA ZABUNI | MAELEZO YA HUDUMA | TAREHE YA KUANZA KWA ZABUNI | MKUTANO UNAOTANGULIA ZABUNI | TAREHE YA MWISHO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KP1/9A.2/OT/019/ICT/22-23 | Ununuzi wa huduma za usaidizi na utunzaji wa mfumo wa usimamizi wa nakala na rekodi za kibiashara-EDRMS (Case 360) | Jumatano 14.12.2022 | N/A | Jumatano 27.12.2022 saa 10.00 a.m. |
| 2. | KP1/9A.3/OT/14/22-23 | Usambazaji wa vyombo na vifaa kwa ukaguzi wa huduma za kibiashara & mauzo na kiufundi | Jumatano 14.12.2022 | N/A | Alhamisi 05.01.2023 saa 10.30 a.m. |
| 3. | KP1/9A.2/OT/020/ICT/22-23 | Utoaji wa usaidizi na utunzaji wa kila mwaka kwa IP PBX na leseni za usajili wa kila mwaka | Alhamisi 15.12.2022 | N/A | Jumatano 04.01.2023 saa 10.00 a.m. |
| 4. | KP1/9A.3/OT/17/22-23 | Usambazaji wa HT Fittings, Surge Arrester, Terminations Joints, Lugs na Service Turrets | Alhamisi 15.12.2022 | N/A | Jumatano 18.01.2023 saa 10.30 a.m. |
| 5. | KP1/9A.4/OT/TPT/03/22-23 | Kazi za kukarabati na utengenezaji zilizopendekezwa katika karakana ya Transport Central Workshop (Ruaraka) | Alhamisi 13.12.2022 | Jumatatu 09.01.2023 at 10.00 a.m. **(Ukumbi Ruaraka, Transport Workshop Boardroom)** | Ijumaa 20.01.2023 saa 10.00 a.m. |

Nakala za zabuni zilizo na mahitaji ya zabuni zilizo hapo juu zinaweza kupatikana kutoka kwenye tovuti ya Kenya Power **(www.kplc.co.ke)** kuanzia **tarehe zilizoonyeshwa hapo juu.**

**MENEJA MKUU**
**USAMBAZAJI NA USAFIRISHAJI**

**www.kplc.co.ke**

DIAL *977# | Access Kenya Power services fast and easy

www.kplc.co.ke @Customercare.kplc.co.ke Kenya Power
@KenyaPower 97771 0703-070 707, 0732-170 170






# KMA yasaka vyombo vya baharini visivyosajiliwa kuinua usalama

**NA EMMANUEL MASHA NA SIRONIK WAITHERA (KNA)**

MAMLAKA ya shughuli za Baharini nchini (KMA), imeanzisha msako dhidi ya vyombo vya usafiri wa majini, ambavyo havijasajiliwa na kupewa leseni ya kuhudumu katika maji ya humu nchini.

Msimamizi wa KMA eneo la Pwani Bw Alex Munga, alisema msako huo unalenga kuhakikisha kuwa tahadhari za kiusalama zimechukuliwa. Bw Munga aliwataka wanaomiliki vyombo hivyo kuvisajili na kuvichukulia leseni kutoka kwa mashirika husika, kabla ya kuyaendesha majini.Licha hayo alieleza kuwa, KMA itakumbatia sera itakayowaruhusu watakaopatikana na makosa ya vyombo vyao kuelea bila leseni, havipitii katika njia ya kawaida ya mahakamani.Alieleza kuwa KMA itawapa watakaopatikana wakiendesha vyombo hivyo bila leseni, muda wa kukata leseni hizo ndani ya muda utakaowekwa..“Ili watu wengi wafuate kanuni, KMA na afisi ya mkuu wa mashtaka (ODPP) zitashirikiana kupinda sheria ili watakaopatikana wakiendesha vyombo vya majini bila leseni watatia saini makubaliano,” alisema. Makubalianao hayo yatakuwa ya kukubali kufuata sheria ya usajili huo kwa muda utakaokuwa umetengwa, badala ya njia ya mahakama,” alisema Bw Mung’a. Akizungumza na wanahabari katika Mbuga ya wanyama wa majini ya kitaifa ya Malindi baada ya msako ulionasa wamiliki watatu wa vyombo vya majini visivyosajiliwa,, Munga alisema msako huo haunuiwi kunyanyasa wamiliki wa vyombo na wahudumu.

**3**

**Wamiliki wa vyombo ambavyo havijasajiliwa**

“Msako huu haunuiwi kunyanyasa mtu yeyote, lakini ni wa kuhimiza watu kusajili vyombo vyao. Haulengi vyombo vya wavuvi au watalii, lakini vyombo vyote vinavyohudumu nchini,” alisema. Alisema kwamba mamlaka hiyo inataka kutambua na kufanya wamiliki wa vyombo hivyo kuwajibika na kwa hili kuwezekana, wamiliki wote wa vyombo vya baharini lazima wasajiliwe na KMA na kupata leseni wanazotakiwa ili kuhudumu. Alisema KMA ndiyo mamlaka iliyo na jukumu la kusajili vyombo vya baharini lakini hili vyombo hivyo viweze kuhudumu, ni lazima vipate leseni kutoka kwa mashirika husika.


REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA UTALII, WANYAMAPORI NA TURATHI

***Idara ya Utalii***

## TANGAZO LA MWALIKO WA ZABUNI

Wizara ya Utalii, Wanyamapori na Turathi, Idara ya Utalii inawaalika wazabuni waliohitimu kutoa huduma zifuatazo: -

| NO | NAMBA YA TENDA | MAELEZO | AINA | KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MOT/04/2022-2023 | Zabuni ya Uchapishaji wa Usanifu, Usambazaji na utoaji wa Kalenda kwa Idara ya Utalii | Wazi | Tarehe 23 Januari 2023 saa 11.00 asubuhi |

1. Idara ya Utalii inakaribisha zabuni kutoka kwa wagombeaji wanaostahiki kwa Usanifu, Uchapishaji, Usambazaji na Uwasilishaji wa Kalenda.
2. Wazabuni wanaostahiki (uthibitisho wa usajili unahitajika) wanaweza kupakua seti kamili ya hati ya zabuni kutoka kwa tovuti ya Idara ya Jimbo kwa Utalii: **www.tourism.go.ke** au tovuti ya Hazina **www.supplier.treasury.go.ke** ***bila malipo yoyote***. Wazabuni wanaopakua hati wanapaswa kujisajilisha na Idara kupitia Barua pepe: **procurement@tourism.go.ke** ili kupata ufafanuzi wowote au nyongeza iliyotolewa.
3. Utoaji wa zabuni utafanywa chini ya Mbinu ya Ushindani ya Kitaifa kwa kutumia hati sanifu ya zabuni. Zabuni iko wazi kwa Wazabuni wote wenye sifa na nia.
4. Nyaraka za zabuni zilizokamilishwa zinapaswa kuwasilishwa zikiambatana na dhamana ya zabuni iliyotolewa na Benki ya Biashara inayoheshimika au Kampuni ya Bima iliyoidhinishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kwa kiasi cha **KES 100,000 (shilingi laki moja pekee)**. Dhamana ya zabuni itakuwa halali kwa muda wa siku mia moja na arobaini (140) kutoka tarehe ya ufunguzi wa zabuni. Kushindwa kutoa dhamana ya zabuni katika muundo sahihi, chanzo sahihi, thamani sahihi na kipindi cha uhalali kutasababisha ombi la mzabuni kufutiliwa mbali.
5. Mzabuni ataratibu kurasa zote za hati za zabuni zilizowasilishwa kwa kufuatana.
6. Nyaraka za Zabuni Zilizokamilishwa, Halisi na Nakala katika bahasha zilizofungwa, zilizoandikwa nambari ya zabuni MOT/04/2022-2023 za Uchapishaji, Usambazaji na Uwasilishaji wa Kalenda na zisizo na dalili zozote za mzabuni zinapaswa kushughulikiwa kwa: -

   **KATIBU MKUU**
   **WIZARA YA UTALII, WANYAMAPORI NA TURATHI**
   **IDARA YA UTALII**
   **S.L.P 30027-00100**
   **NAIROBI**

   na kuwekwa kwenye Sanduku la Zabuni kwenye Orofa ya 8 katika Jengo la Hazina ya Utalii, Nairobi ili ipokewe tarehe **23 Januari, 2023 saa 11.00 asubuhi** au kabla. Zabuni zilizowasilishwa zitafunguliwa hadharani katika Chumba cha Mikutano cha orofa ya 9, Jengo la Hazina ya Utalii, punde tu baada ya tarehe na wakati wa kufunga uliotajwa hapo juu mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaochagua kuhudhuria.
7. Zabuni zitakazochelewa zitakataliwa.
8. Bei zilizonukuliwa lazima zijumuishe VAT na Ushuru wote wa Serikali, lazima ziwe katika Shilingi za Kenya, na lazima zisalie kuwa halali kwa siku mia moja arobaini (140) kuanzia tarehe ya kufunguliwa kwa zabuni.
9. Serikali inahifadhi haki ya kukataa zabuni yoyote na inaweza kubatilisha mchakato wa zabuni au kukataa zabuni zote wakati wowote kabla ya kutolewa kwa kandarasi bila hivyo kuwa na dhima yoyote kwa mzabuni au wazabuni walioathirika.
10. Anwani ya kupata maelezo zaidi kuhusu zabuni ni **procurement@tourism.go.ke**, na Jengo la Hazina ya Utalii, Nairobi, orofa ya 8, Chumba 820.

**KATIBU WA WIZARA**
**WIZARA YA UTALII, WANYAMAPORI NA TURATHI**
**IDARA YA UTALII**
**S.L.P 30027,00100**
**NAIROBI.**

ISO 9001:2008 Certified.
KENYA VISION 2030



KAA Kenya Airports Authority

## TENDER ADVERTISEMENT NOTICE

The Kenya Airports Authority invites sealed tenders from eligible firms for the following tenders: -

| REFERENCE NUMBER | TENDER DESCRIPTION | PRE-BID MEETING/ SITEVISIT-OPTIONAL | CLOSING/ OPENING DATE |
|---|---|---|---|
| KAA/OT/WAP/0091/2022- 2023 | Re-Tender for Provision of Cleaning Services for General Areas, Toilets at Wilson Airport.<br>***(Eligibility Duly Registered Persons Living with Disability only (PWD's)*** | The mandatory site visit has been scheduled on 25th January 2023 at 11:00am | 31/01/2023 at 11.00 a.m. |
| KAA/OT/WAP/0092/2022- 2023 | Provision of Environmental Management Services at Wilson Airport.<br>(Grass cutting, vegetation control, gardening, afforestation, buffer zone, drainage, cleaning of all paved areas and garbage collection)<br>***(Eligibility Duly Registered Youth Group and Women Enterprises)*** | The mandatory site visit has been scheduled on 26th January 2023 at 11:00am | 31/01/2023 at 11.00 a.m. |
| KAA/OT/UKUNDA/0093/2022-2023 | Re-Tender for Provision of Cleaning Services at Ukunda Airstrip.<br>***(Eligibility Duly Registered Youth Group, Women and People living with Disability Owned Enterprises)*** | Bidders will be required to seek through the email address, **tenders@kaa.go.ke** for prior appointment before visiting the sites. | 1/02/2023 at 11.00 a.m. |
| KAA/OT/KIA/0094/2022-2023 | Provision of Cleaning Services at Kisumu International Airport.<br>***(Eligibility Duly Registered Youth Group, Women and People living with Disability Owned Enterprises)*** | Bidders will be required to seek through the email address, **tenders@kaa.go.ke** for prior appointment before visiting the sites. | 1/02/2023 at 11.00 a.m. |
| KAA/OT/HQS/0095/2022-2023 | Framework Contract for Procurement of Various Tyres for Heavy Equipment/Plant, Motor Vehicles and Motor Cycles for Kenya Airports Authority. | N/A | 2/02/2023 at 11.00 a.m. |
| KAA/OT/MLD/0096/2022-2023 | Provision of Cleaning Services for General Areas, Washrooms, Pest Control, Fumigation and Waste Management at Malindi Airport.<br>***(Eligibility Duly Registered Youth Group, Women and People living with Disability Owned Enterprises)*** | Bidders will be required to seek through the email address, **tenders@kaa.go.ke** for prior appointment before visiting the sites. | 2/02/2023 at 11.00 a.m. |

Information on these tender notices and documents detailing the requirements, tendering procedures and guidelines should be downloaded from our website at **https://www.kaa.go.ke/corporate/procurement/** or **https://suppliers.kaa.go.ke/irj/portal** or Public or Procurement Information Portal at **www.tenders.go.ke** ***free of charge.***

Bidders are advised to note that bidding process for the tenders is through our online tender portal at **https://suppliers.kaa.go.ke/irj/portal.** For any information or clarifications, please contact us through our email, **tenders@kaa.go.ke**

Canvassing for the tender by the tenderer or by proxy shall lead to automatic disqualification of their tender.

**MANAGING DIRECTOR/CEO**

KENYA VISION 2030

KOMESHA COVID-19

" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"




# Kiwanda cha Sh800 milioni cha kubadilisha maji taka kujengwa

**NA EMMANUEL MASHA (KNA)**



**Gavana wa KIlifi, Gideon Mung'aro ahutubia waumini wa kanisa la JCC, mjini Malindi wakati wa ibada ya Jumapili.** PICHA: EMMANUEL MASHA

Serikali ya kaunti ya Kilifi, itajenga kiwanda cha kubadilisha maji taka kwa gharama ya Sh800 milioni mjini Malindi kutengeneza matofali ya makaa kutatua shida ya kawi katika eneo la Pwani Kaskazini.

Akitoa tangazo hilo, Gavana wa Kilifi Gideon Mung'aro alisema kwamba hivi karibuni atazindua kiwanda kinachojengwa eneo la

Sabaki, kaunti ndogo ya Malindi kwa ufadhili kutoka Benki ya Dunia.

Mung'aro alisema kwamba kiwanda hicho kitatumia taka ya binadamu kutoka vyoo katika miji ya Malindi na Watamu kutengeneza makaa ya mawe yatakayouziwa wakazi na kupunguza kutegemea makaa ya miti kunakolaumiwa kwa uharibifu wa mazingira.

Gavana alisema kwamba makaa hayo yatatengenezwa kutoka kwa mchanganyiko wa rojorojo, maganda ya nazi na matawi, akiongeza kuwa mradi huo ni sehemu ya ajenda ya serikali yake kusafisha mji wa Malindi na mazingira yake kwa lengo la kufufua sekta ya utalii.

"Malindi unafaa kuwa safi. Tayari tuko na washirika wa maendeleo na katika muda wa wiki moja au mbili tutakuwa tukizindua mradi mkubwa wa usafi Sabaki ambao tutatengeneza makaa ili watu waache kukata miti," alisema.

Mung'aro alisema kwamba serikali yake, kwa usaidizi wa washirika wa maendeleo, imeanza ujenzi wa vyoo vilivyopangwa vyema katika miji ya Malindi na Watamu, mradi ambao utagharimu takriban Sh120 milioni.

Gavana alisema kwamba vyoo hivyo vya kisasa, vitakuwa na miongoni mwa huduma zingine, bafu ya kisasa zilizo na vifaa vya kisasa.

"Ninataka kusema wazi hapa kwamba, vyoo hivi vitakapokuwa tayari, vitasimamiwa na makundi ya vijana na wanawake. Hii pia itakuwa njia nyingine

> Ningependa kusema kuwa pindi tu vyoo hivi vitakapokuwa tayari vitasimamiwa na vijana na kinamama." -Mung'aro

ya kuunda nafasi za ajira," alisema.

Alisema kwamba anataka kuimarisha mfumo wa kuondoa maji katika mji wa Malindi ambao alisema umekuwa tatizo maendeleo ya mji huo wa kitalii na pia kumaliza shida ya kila mara ya uhaba wa maji.

" Katika siku za kwanza 100 nikiwa ofisini, nilianzisha usambazaji wa dawa katika vituo vyetu vyote vya afya na sasa tumemaliza shida ya ukosefu wa dawa. Shida tuliyo nayo sasa ni mahali pa kuhifadhi dawa, tumelazimika kuziweka katika wodi," alisema.

REPUBLIC OF KENYA

NTSA Keep our roads safe

**National Transport and Safety Authority**

## TANGAZO LA KAZI

Mamlaka ya Kitaifa ya Usafiri Salama Barabarani (NTSA) ni Shirika la Serikali lililoanzishwa kupitia Sheria ya Bunge; Sheria Namba 33 ya tarehe 26 Oktoba 2012. Mamlaka imepewa jukumu la kusimamia ipasavyo sekta ndogo ya usafiri wa barabarani, kupunguza ajali za barabarani na kupoteza maisha kutokana na hali hiyo.

Kwa mujibu wa jukumu hili, Mamlaka inataka kuajiri watu wenye ari ya juu, wenye dira na mwelekeo wa matokeo kujaza nafasi zifuatazo:

| S/No. | Nafasi | Gredi | Idadi ya Nafasi | Marejeleo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Meneja, Uhasibu wa Fedha na Kuripoti | NTSA 4 | 1 | NTSA/01/2023/02 |
| 2. | Afisa Mkuu wa Fedha | NTSA 6 | 1 | NTSA/01/2023/03 |
| 3. | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | NTSA 6 | 1 | NTSA/01/2023/04 |
| 4. | Afisa Mkuu – Usimamizi wa Mradi na Uhamasishaji wa Rasilimali | NTSA 6 | 1 | NTSA/01/2023/05 |
| 5. | Afisa Ukaguzi II – Mifumo | NTSA 8 | 1 | NTSA/01/2023/06 |

1. **MENEJA, UHASIBU WA FEDHA & KURIPOTI (DARAJA LA NTSA 4) – KUMB NTSA/01/2023/02**
Kuripoti kwa Naibu Mkurugenzi, Fedha mwenye kazi anawajibika kwa uhasibu wa kifedha na kazi ya kuripoti ya idara ya fedha.

2. **AFISA MKUU WA FEDHA (DARAJA LA NTSA 6) – KUMB NTSA 01/2023/03**
Kuripoti kwa Meneja, Uhasibu wa Fedha na Kuripoti mwenye kazi atawajibika kwa miradi na usimamizi wa mali.

3. **MKAGUZI MKUU WA NDANI (DARAJA LA NTSA 6) – KUMB NTSA 01/2023/04**
Kuripoti kwa Meneja, Ukaguzi wa Ndani mwenye kazi atawajibika kukagua na kutathmini mfumo wa udhibiti wa ndani, kutathmini utoshelevu wao, ufanisi na kupendekeza mapendekezo ya uboreshaji wao.

4. **AFISA MKUU- USIMAMIZI WA MRADI NA UHAMASISHAJI WA RASILIMALI (DARAJA LA NTSA 6) – KUMB: NTSA 01/2023/05**
Kuripoti kwa Meneja Mkakati na Mipango ya Biashara, mwenye kazi atasaidia katika Uratibu wa Mradi na Uhamasishaji wa Rasilimali. Afisa pia atafanya mazoezi ya Ufuatiliaji na Tathmini ya programu za Mamlaka pamoja na kuandaa na kuwasilisha ripoti za mara kwa mara.

5. **AFISA UKAGUZI II – MIFUMO (DARAJA LA NTSA 8) – KUMB NTSA 01/2023/06**
Kuripoti kwa Afisa Mkuu wa Ukaguzi – Mifumo, mwenye kazi atawajibika kwa maendeleo na utekelezaji wa mpango wa ukaguzi wa kila mwaka wa Mifumo ya Taarifa.

Wagombea wanaovutiwa na nafasi hiyo hapo juu wanatarajiwa kutimiza mahitaji na uzoefu yaliyoelezwa katika yetu tovuti **www.ntsa.go.ke.**

Maombi yanapaswa kutumwa kwenye Mapokezi ya Ofisi Kuu ya Mamlaka, 316 Upper Hill Chambers Ground floor, 2nd Ngong Avenue, au kutumwa kwa;

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Kitaifa ya Usafiri Salama Barabarani,**
**P.O. Box 3602-00506, Nairobi**

Maombi yote yasipokewe kupita saa 5.00 jioni, Jumanne, tarehe 31 Januari 2023

***NTSA ni mwajiri aliyejitolea kutoa nafasi sawa na usawa wa kijinsia. Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu wanahimizwa kutuma maombi. Tafadhali kumbuka kuwa wagombea walioorodheshwa pekee ndio tutawasiliana nao. Ombi la yeyote atakayepatikana akidangaya litafutiliwa mbali.***

***www.ntsa.go.ke***

REPUBLIC OF KENYA

UPPER TANA NATURAL RESOURCES MANAGEMENT PROJECT UTaNRMP Poverty Reduction Through Sustainable NRM

IFAD Investing in rural people

## WIZARA YA MAJI, USAFI NA UNYUNYIZAJI

### IDARA YA MAJI NA USAFI

**MRADI WA USIMAMIZI WA MALIASILI WA CHEMICHEMI YA UPPER TANA (UTaNRMP)**
**P.O. Box 996-60100 Embu; Tel 068 22 31376; Email:utanrmp@gmail.com www.utanrmp.or.ke**

## OMBI LA MWALIKO WA ZABUNI
### (Washauri Binafsi)

Serikali ya Kenya imepokea msaada wa kifedha kutoka kwa Hazina ya Kitaifa ya Kustawisha Kilimo (IFAD) kufadhili Mradi wa Usimamizi wa Maliasili wa Chemichemi ya Upper Tana na inatarajia kutumia sehemu ya mapato kwa ajili ya utafutaji wa huduma za ushauri zinazotolewa na washauri binafsi kama sehemu ya timu ya kufanya Tathmini ya Kukamilisha Mradi (PCR)

Mradi wa Usimamizi wa Maliasili wa Chemichemi ya Upper Tana (UTaNRMP) sasa unawaalika Washauri Binafsi wanaostahiki chini ya maeneo ya utaalamu yafuatayo: -

1. **Mtaalamu wa Uchumi na Fedha - UTaNRMP/PCR/001/2022-23**
2. **Mtaalamu wa Maliasili/Mazingira - Kumb Na. UTaNRMP/PCR/002/2022-23**
3. **Mtaalamu wa Maji - UTaNRMP/PCR/003/2022-23**
4. **Mtaalamu Fiduciary - Namba ya Kumb: UTaNRMP/PCR/004/2022-23**
5. **Mtaalamu wa Ulengaji, Jinsia na Vijana - Ref Na. UTaNRMP/PCR/005/2022-23**
6. **Mtaalamu wa Uboreshaji wa Mfumo wa Kilimo- Ref Na. UTaNRMP/PCR/006/2022-23**

Washauri wanaovutiwa wanaweza kupata maelezo zaidi kuhusu washauri, jinsi ya kutuma maombi na taratibu za kuorodheshwa katika **www.utanrmp.or.ke**, na **www.water.go.ke**

Hati za Ombi Lililokamilishwa la Maonyesho ya Nia (REOI) zilizo katika bahasha iliyofungwa wazi na yenye alama ya mtaalam husika na nambari ya kumbukumbu zinapaswa kushughulikiwa na kutumwa kwa:

**Mratibu wa Mradi,**
**Mradi wa Usimamizi wa Maliasili wa Chemichemi ya Upper Tana,**
**P.O BOX 996-60100**
**Simu: 254-68-2231376/2231517**
**EMBU**

au kuwekwa kwenye Sanduku la Zabuni lililo kwenye lango kuu la ofisi za EMBU West Water zilizopo Barabara ya Embu-Meru mkabala na Shule ya Msingi ya Kangaru DEB au ichapishwe ili kufikia anwani iliyo hapo juu mnamo **7 Februari 2023** au kabla, kabla ya saa **11:00 asubuhi.**

Ufunguzi utafanyika tarehe **7 Februari 2023** saa **11:00 asubuhi** mbele ya wazabuni au wawakilishi wao wanaochagua kuhudhuria katika ofisi za Mradi, Kituo cha Nyaraka cha MKEPP. Zabuni za kielektroniki na mawasilisho yaliyochelewa hayatakubaliwa bila kujali hali.

KENYA VISION 2030

# Serikali yasisitiza itaendelea kusaidia sekta inayotatizika ya uandishi habari

NA JERRY ABUGA (MEDIA COUNCIL OF KENYA)



Serikali imehakikishia wanahabari kwamba itabuni mazingira bora kwa sekta hiyo kufanya kazi yake kwa kuweka sheria ya kuiwezesha kutimiza malengo yake.

Katibu wa Utangazaji na Mawasiliano katika Wizara ya Habari, Mawasiliano na Uchumi Dijitali, Profesa Edward Kisiang'ani alipongeza Baraza la kusimamia uanahabari kwa kuongoza juhudi za kubadilisha sheria za zamani kuhusu shughuli za wanahabari nchini ili kupatia nchi sera yenye nguvu ya kuongoza shughuli za wanahabari.

"Serikali inatambua nafasi muhimu ya uhuru wa wanahabari. Tutasaidia wanahabari kutekeleza jukumu lao katika kuchangia masuala ya maslahi ya kitaifa kupitia ripoti sahihi," alisema katibu huyo.

Profesa Kisiang'ani aliyekuwa akizungumza katika mkutano wa kuchunguza mkakati ulioandaliwa na Baraza la Wanahabari la Kenya (MCK) alisema kwamba serikali itashirikiana kwa karibu na wanahabari kushinikiza utoaji wa huduma na kutimiza ajenda yake ya maendeleo akisema kwamba nchi zilizo na vyombo vya habari vinavyonawiri vina ajenda nzuri ya maendeleo.

"Hatuna mpango wa kupiga vita yeyote, ikiwemo vyombo vya habari kwa kuwa uhuru wa uanahabari umehakikishwa katika Katiba. "Badala yake, tutashirikiana na wadau wote kuweka sheria ambazo zitanyoosha shughuli za uanahabari nchini na Baraza la Wanahabari linapaswa kuwa msitari wa mbele katika juhudi hizi," alisema Katibu huyo wa wizara.

Hata hivyo, alionya mashirika ya habari dhidi ya kuwanyanyasa wafanyakazi hasa kufuatia kuachishwa kazi na kukatwa mishahara katika vyombo vya habari nchini hivi majuzi.

"Wamiliki wa vyombo vya habari vya kibinafsi hawafai kuruhusiwa kutishia uwepo wa uanahabari kupitia mbinu mbaya za biashara. Wafanyakazi katika vyombo vya habari lazima walindwe kutoka biashara zinazowatesa".

Alifichua kwamba serikali, kupitia Shirika la Matangazo ya Serikali (GAA), imejitolea kusaidia vyombo vya habari, na akaongeza kuwa kufikia sasa imetoa pesa za kulipa madeni ambayo shirika linadaiwa.

"Miongoni mwa Sh 1.2 bilioni zinazodaiwa na wanaotoa matangazo, kufikia sasa tumelipa kampuni za habari Sh244 milioni. Hata hivyo, hakuna kampuni ya habari imetangaza hilo na nyingi zinaendelea kufuta kazi wafanyakazi wao. Hii sio haki na haifai kuruhusiwa," alisema.

Alihimiza Baraza La Habari Kenya (MCK) kuzungumza na wamiliki wa vyombo vya habari wakumbatie miundo ya biashara na utaalamu wa kuripoti na pia akarai mashirika ya habari kukumbatia ubunifu katika shughuli zao yanapokumbatia dijitali.

Profesa Kisiang'ani pia alihimiza Baraza la Habari Kenya kutekeleza jukumu lake la kuinua utaalamu katika uanahabari.

"Lazima mdhibiti, Baraza la Habari linapaswa kuhakikisha wanahabari wanatoa ripoti sahihi. Tume ya Malalamishi kuhusu uanahabari inapaswa kutambua ukiukaji wa Kanuni za Mwongozo wa Uanahabari Kenya na kuongoza wanahabari ipasavyo," alisema.

Katibu wa Wizara alishauri wanahabari kudadisi manifesto ya serikali na kuripoti kwa usawa masuala kuhusu Kilimo, Biashara Ndogo na za Kati, nyumba na makao, huduma za afya na mfumo mkubwa wa dijitali, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

"Serikali imejitolea kuwa na ushirikiano na wanahabari ili kuimarisha utoaji wa huduma na kiwango cha maisha kwa Wakenya wote.

"Tuwe na majadiliano chanya na ninahimiza vyombo vya habari kuepuka kuunga mirengo ya kisiasa kwa kuwa serikali hubadilika. Wanahabari wanafaa kutekeleza jukumu lao bila kuegemea upande wote," alisema Profesa Kisiang'ani.

Afisa Mkuu Mtendaji wa Baraza la Habari la Kenya David Omwoyo alisema kwamba Baraza hilo limeanza kuchunguza Mpango wake wa Mkakati kutokana na mabadiliko ya dijitali katika habari.

Alisema kwamba kuwekwa huru kwa uanahabari kumesababisha ukuaji mkubwa wa habari na akahimiza mashirika ya habari kuzingatia utaalamu.

**244M**

**Pesa zilizotolewa kwa vyombo vya habari**


REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA MAJI, USAFI NA UNYUNYIZAJI

### IDARA YA UNYUNYIZAJI

**MRADI WA USALAMA WA MAJI NA USTAHIMILI WA HALI YA HEWA KENYA (KWSCRP)**

| MRADI NA: | P117635 | MKOPO NA.: | 5268-KE |
|---|---|---|---|

**HUDUMA ZA USHAURI – UTEUZI MASHIRIKA**

**OMBI LA MWALIKO WA ZABUNI (REOI)**
**LA**
**MSHAURI WA UNAKILI NA UTATHMINI**

| ZABUNI NAMBA.: | MOWS/KWSCRP-1/001/2022-2023 |
|---|---|

1. Serikali ya Kenya imepokea ufadhili kutoka kwa Benki ya Dunia kugharamia **Mradi wa Usalama na Kustahimili Hali ya Hewa Kenya** na inakusudia kutumia sehemu ya mapato kutoka kwa ufadhili huu kwa malipo ya **Mshauri wa Unakili na Utathmini** wa Mradi wa Unyunyiziaji Maji wa Lower Nzoia.

2. Lengo kuu la Huduma za Ushauri ni kutoa hesabu kamili na ya kimfumo ya utendaji na matokeo ya mradi kwa kutathmini matokeo, umuhimu na ufanisi dhidi ya malengo yaliyokubaliwa, na viashiria muhimu vya utendaji vilivyoelezwa katika mfumo wa matokeo ya mradi. Hii itakuwa hati katika hati ya ICR ambayo hutoa akaunti ya serikali na kulisha moja kwa moja kwenye ripoti ya Benki yenyewe ya ICR. Kwa hivyo, malengo ya msingi ya kazi hii ni kama ifuatavyo.

   a) Fanya tathmini ya mradi ili kubainisha kiwango ambacho KWSCRP imefikia Mradi Malengo ya Maendeleo (PDOs) na viashirio vya athari vinavyohusiana. Miongoni mwa mambo mengine, tathmini inapaswa:

      i. Hutathmini na kuorodhesha shughuli na matokeo ya shughuli.

      ii. Tathmini matokeo na matokeo ya muda mrefu ya operesheni dhidi ya malengo yaliyokubaliwa; kwa kuzingatia kutoa ushahidi wa mafanikio ya malengo ya mradi na mchango wa shughuli zinazosaidiwa na matokeo kwa matokeo ya maendeleo ya mradi;

      ii. Inatathmini uendelevu wa matokeo, kama mradi haukushughulikia au kuchukua baadhi ya shughuli, je, hizi zitaendelezwaje?

      iv. Tathmini mambo muhimu na matukio yanayohusu Benki, serikali ya Kenya, KfW, washirika wengine, na mazingira ya nje (ikiwa ni pamoja na nje ya udhibiti wa wadau wa utekelezaji) wakati wa maandalizi, wakati wa kuingia na utekelezaji, ambayo yaliathiri utendaji na matokeo.

      v. Kukosoa utendaji wa serikali (ikiwa ni pamoja na Vitengo vya Utekelezaji wa Miradi - PIUs) wakati wa maandalizi na utekelezaji wa mradi kwa msisitizo maalum juu ya mafunzo ambayo yanaweza kusaidia katika siku zijazo; na

      vi. Kosoa utendaji wa Benki.

      vii. Eleza mipangilio ya uendeshaji wa mradi wa baadaye (au miradi kama hiyo ya ufuatiliaji).

   b) Hati kwa utaratibu na kisayansi hali ya sasa ya viashiria muhimu vya mradi, na maalum mkazo katika viashiria vya kiwango cha matokeo, na uendelevu wa matokeo.

   c) Jaza kiolezo cha ndani cha mradi wa ICR kama itakavyotolewa na Mtaalamu wa Usimamizi wa Maarifa wa KWSCRP.

3. Kwa Masharti ya kina ya Marejeleo ya kazi hii ikijumuisha malengo mahususi, upeo wa majukumu, ufunguo zinaweza kuwasilishwa, muda, uwezo, sifa na mahitaji mengine, tafadhali tembelea tovuti ya Mradi: **www.tender.go.ke**

4. Muda wa huduma ya ushauri ni **siku 30** zilozosambazwa katika muda usiozidi miezi 3 tangu tarehe ya kuanza.

5. Wizara ya Maji, Usafi na Unyunyizaji sasa inakaribisha mashirika ya ushauri yanayostahiki ("Washauri") ili kuonyesha nia yao ya kutoa Huduma. Washauri Wanaovutiwa wanapaswa kutoa habari inayoonyesha kuwa wana sifa zinazohitajika na uzoefu unaofaa kutekeleza Huduma. Vigezo vya uorodheshaji mi kama yafuatayo:
   **a) Umuhimu na ufaafu wa biashara ya msingi ya mwombaji kwa kazi hiyo.**
   **(b) Angalau uzoefu wa miaka kumi (10) katika Ufuatiliaji, Tathmini na Utafiti. Kampuni lazima iwe imefanya angalau miradi mitano (5) ya Ufuatiliaji, Tathmini na Utafiti nchini Kenya au Afrika Mashariki.**
   **(c) Awe na uzoefu wa kufanya tathmini ya mradi hasa katika sekta ya kilimo na maji/umwagiliaji**
   **d) Ustadi bora wa kuandika ripoti unaothibitishwa na ripoti tatu (3) za hivi majuzi za maendeleo zenye ukubwa sawa**
   **(e) Mshauri lazima awe na ujuzi katika upimaji wa ubora na upimaji na**
   **(f) Mahiri katika programu za uchanganuzi wa data kama vile SPSS, Epi-info au STATA**

***Kumbuka: i) Kampuni inapaswa kutoa ushahidi ili kuunga mkono tajriba/mgawo uliotajwa na sambamba marejeleo ya mteja/na au vyeti vya kukamilika.***
***ii) Data ya wataalam muhimu (CV) haitatathminiwa katika hatua hii.***

6. Washauri wanaovutiwa wanashauriwa kuangalia kwenye aya ya 1.9 ya ***Miongozo ya Benki ya Dunia: Uteuzi na Ajira ya Washauri [chini ya Mikopo ya IBRD na Mikopo na Ruzuku za IDA] na Wakopaji wa Benki ya Dunia, Januari 2011 iliyorekebishwa Julai 2014*** ("Miongozo ya Mshauri"), kuweka sera ya Benki ya Dunia kuhusu mgongano wa maslahi.

7. Mashirika yanaweza kushirikiana kwa njia ya ubia au ushauri mdogo ili kuboresha sifa zao. Jukumu la kila mshirika katika chama lazima lielezwe wazi.

8. Mshauri atateuliwa kwa mujibu wa ***Mbinu ya Sehemu ya Sifa ya Mshauri (CQS)*** iliyowekwa katika ***Miongozo ya Benki ya Dunia: Uteuzi na Ajira ya Washauri [chini ya Mikopo ya IBRD na Mikopo & Ruzuku ya IDA] na Wakopaji wa Benki ya Dunia, Januari 2011 iliyorekebishwa Julai. 2014*** ("Miongozo ya Mshauri")

9. Washauri wenye nia wanaweza kupata maelezo zaidi muhimu katika anwani iliyo hapa chini wakati wa saa za kazi kati ya saa 0900 hadi 1600 kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa bila kujumuisha saa za chakula cha mchana (1300 hadi 1400Hrs) na sikukuu za umma.

10. Maelezo yaliyokamilishwa ya hati za riba kwa maandishi katika nakala tatu (3) lazima ziwasilishwe kwenye **Sanduku la Zabuni** kwenye **Orofa ya Chini, Maji House** au zitumwe kwa barua pepe au anwani iliyo hapa chini ili zipokewe tarehe **31 Januari 2023** saa **10.00 asubuhi** saa za Afrika Mashariki. Kwa maelezo ya riba yatakayowekwa kwenye sanduku la zabuni, vifurushi vinapaswa kuwekewa alama wazi: **"MSHAURI WA UNAKILI NA UTATHMINI KWA MRADI WA UNYUNYIZAJI MAJI WA LOWER NZOIA**; NAMBA YA MKATABA: **MOWSI/KWSCRP-1/001/2022-2023** itumwe kwa:

**Katibu wa Wizara**
**Wizara ya Maji, Usafi na Unyunyizaji**
**Idara ya Unyunyizaji**
**Mradi wa Usalama na Kustahimili Hali ya Hewa Kenya,**
**Maji House Orofa ya 5, Chumba Na. 513/544/547, Barabara ya Ngong,**
**P.O. Box 49720-00100, Nairobi.**
**Simu: +254 20 2716103 Ext. 42366/42335/42260**
**Barua pepe: procurement@kwscrp.org**

KENYA VISION 2030




" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"




# Serikali yakumbatia hatua stahimilivu za kukabili athari za ukame mrefu

**NA BEN MWENDWA (PCO)**

Serikali ya Kitaifa na serikali za kaunti zimeungana katika juhudi za kuokoa maisha huku nchi ikikabiliwa na hali mbaya baada ya mvua kufeli tena.

Hii ni kulingana na Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Maeneo Kame na Maendeleo ya Kikanda Bi Rebecca Miano.

Akishukuru hatua muhimu inayotekelezwa na washirika wa maendeleo, sekta ya kibinafsi, wadau wasio wa serikali na wasamaria wema Wakenya, Miano anasema kwamba serikali imeongeza juhudi za kukabili ukame ili kukinga maisha na shughuli za kujikimu za wanaothiriwa na ukame.

Akihutubia wanahabari katika ofisi yake Nairobi, Miano alihakikishia taifa kwamba serikali inathibiti Hali na itafanya kila iwezalo kuokoa maisha.

"Tumetambua kaunti zilizoathiriwa, kaunti ndogo na wadi ambazo zimeathiriwa ili kuimarisha misaada. Hatua zinategemea ripoti ya Kamati za

> Serikali inajitolea kuchukua hatua kabambe kuhakikisha tuko tayari kukabiliana na hali yoyote –Miano

Usimamizi za Kaunti (CSGs), ambazo zinasimamiwa na magavana" alisema Miano. Kwa kuitikia mwito wa umma wa kusaidia serikali katika juhudi zake za kushughulikia mahitaji yanayoongezeka ya msaada wa binadamu, Rais William Ruto aliunda Kamati ya Kitaifa inayoongozwa na Sekta ya Kibinafsi kushughulikia ukame. Serikali ilitwika kamati hiyo jukumu la kutafuta pesa za kusaidia juhudi zake za kukabiliana na hali inayoendelea ya ukame. Hii imesaidia serikali kukabili ukame kupitia chakula cha msaada; kutumia pesa waathiriwa; kupima na kutibu wanaoathiriwa na utapia mlo; kusambaza maji kwa malori; kutoa lishe ya mifugo na kununua mifugo.

Waziri alisema kwamba, katika mwezi wa Desemba 2022 pekee kamati hiyo ilisambazia chakula cha msaada familia 14,300 katika kaunti 5 chini ya mpango wa Wakenya Tulindane.

Msaada huo wa chakula ulilenga familia 2,860 katika kaunti ndogo zilizoathiriwa zaidi za Magarini (Kilifi), Mwingi Kaskazini (Kitui), Samburu Mashariki (Samburu), Moyale (Marsabit) na Igembe Kaskazini (Meru).

"Tunashukuru kwa dhati wadau wote na Wakenya ambao wamejitokeza kusaidia na tunahimiza wadau wetu kuungana na serikali kupunguza ukosefu wa uwezo na kuinua usaidizi wetu.

"Nachukua fursa hii kuhakikisha wananchi kwamba serikali imejitolea kujenga ustahilimivu ili kuhakikisha hali yetu ya maandalizi imeshughulikiwa na hakuna mtu atapoteza maisha kutokana na njaa," alisema Waziri.

Wizara hiyo, kupitia Mamlaka ya Taifa ya Kusimamia Majanga inafuatilia kwa karibu hali ya ukame kupitia ushirikiano wa mashirika tofauti yanayotumaini msimu wa mvua za vuli za 2022 kubaini athari zake kwa utoshelevu wa chakula.



Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Maeneo Kame na Ustawi wa Kikanda Bi Rebecca Miano akiwa afisini mwake

REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA MAJI, USAFI NA UNYUNYIZAJI

### IDARA YA MAJI NA USAFI

### MAMLAKA YA KUSTAWISHA MAJI YA NORTH RIFT VALLEY

NORTH RIFT VALLEY WATER WORKS DEVELOPMENT AGENCY
Enhanced Access to Safe Water

## MWALIKO WA ZABUNI

### ZABUNI YA USHINDANI WA KITAIFA

1. Serikali ya Jamhuri ya Kenya kupitia Wizara ya Maji, Usafi na Unyunyizaji imetenga fedhja kwa Mamlaka ya Kustawisha Maji ya Bonde la Ufa (NRVWWDA) kwa ajili ya kuwatafuta wakandarasi wa ujenzi wa Miradi ya Usambazaji Maji ndani ya Eneo lake.

2. Mamlaka sasa inakaribisha zabuni kutoka kwa wazabuni wanaostahiki kwa ajili ya ujenzi wa Miradi ya Kusambaza Maji kama ifuatavyo:

| No | Namba ya Marejeleo ya Zabubni | Maelezo | Uhitimu | Tarehe ya kuzuru eneo kabla ya zabuni | Eneo la kukutana | Tarehe na wakati wa kuwasilisha zabuni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | NRV/GOK/WFS/TUR/2022-23/01 | Uwekaji na Kazi za Kiraia za Mradi wa Kisima wa Nakwamekwi/ Kopeto | Wazi | N/A | N/A | Februari 3, 2023 saa 12:00 mchana |
| 2 | NRV/GOK/BH/UG/2022-23/02 | Uchimbaji, Utayarishaji na Kazi za Kiraia katika Kisima cha Maji cha Kamoret | Wazi | N/A | N/A | Februari 3, 2023 saa 12:00 mchana |
| 3 | NRV/GOK/WP/UG/2022-23/03 | Kazi za Ukarabati na Upanuzi wa Bawa la Maji la Kamoret | Wazi | Januari 20, 2023 saa 10:00 asubuhi | Ofisi za NRVWWDA, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (OAG), Jengo, Barabara ya Furfural, Eldoret | Februari 3, 2023 saa 12:00 mchana |
| 4 | NRV/GOK/WP/EMC/2022-23/04 | Kazi za Ujenzi za Mabwawa Madogo ya Maji ya Chepchor-Muruber | Imetengewa Makundi Maalum (Vijana, Wanawake na Walemavu) | Januari 23, 2023 saa 10:00 asubuhi. | Kituo cha Soko la Chesongoch kando ya Barabara ya Biret-wo-Tot | Februari 3, 2023 saa 12:00 mchana |

3. Mahitaji ya lazima na taarifa za kufuzu ni kama ilivyoelezwa katika nyaraka za zabuni husika.
4. Wazabuni wanaohitajika wanaweza kupata maelezo zaidi kutoka kwa Mamlaka ya Kustawisha Maji ya Bonde la Ufa (NRVWWDA, Afisa Mkuu Mtendaji, kupitia barua pepe **info@nrvwwda.go.ke** au **procurement@nrvwwda.go.ke**
5. Seti kamili ya hati za zabuni kwa Kiingereza zinaweza kupakuliwa kutoka kwa tovuti ya NRVWWDA **www.nrvwwda.go.ke** na **www.tenders.go.ke**, ***bila malipo***. Wazabuni wanaopakua hati za zabuni kutoka kwa tovuti **LAZIMA** wapeleke maelezo yao mara moja kwa **info@nrvwwda.go.ke**, kwa rekodi na ufafanuzi wowote zaidi na nyongeza. na
6. Zabuni zote l**azima** ziambatane na dhamana ya zabuni katika mfumo wa Dhamana ya Benki bila masharti kama ilivyoainishwa katika zabuni husika hati.
7. Zabuni lazima ziwasilishwe kwa anwani iliyo hapa chini mnamo au kabla ya tarehe zilizoainishwa kwenye jedwali hapo juu. Zabuni zilizochelewa zitakataliwa. Zabuni zitafunguliwa hadharani mbele ya wawakilishi wote walioteuliwa wa wazabuni na mtu yeyote anayechagua kuhudhuria katika anwani iliyo hapa chini kwa tarehe husika kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo juu.
8. Ufunguzi wa zabuni utaendana na Miongozo ya PPRA kama ilivyoainishwa kwenye waraka Na. 02/2020 ambayo inaweza kupatikana kutoka kwa wavuti yao **www.ppra.go.ke.**
9. Anwani ya taasisi nunuzi ni kama ifuatavyo;

**Afisa Mkuu Mtendaji,**
**Mamlaka ya Kustawisha Maji ya Bonde la Ufa,**
**Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, (Orofa ya 2),**
**Barabara ya Furfural,**
**Kinyume cha Kitengo cha Mitambo na Usafiri**
**P.O. BOX 1012-30100,**
**Mji wa Eldoret, Kenya.**
**Simu: 254-700 347 896/254-753 347 896;**
**Barua pepe: info@nrvwwda.go.ke**

KENYA VISION 2030

# KNLS, China zatia saini mkataba kuinua utamaduni, lugha asili



**NA MATHEW CHEPKEWEL (MYGOV)**

Huduma ya Taifa ya Maktaba Kenya (KNLS), na ubalozi wa China, Nairobi zimezindua ushirikiano unaonuiwa kuinua utamaduni na lugha za kitaifa za nchi hizo mbili. Akizungumza na MyGov, Afisa Mkuu Mtendaji wa KNLS (CEO) Dkt Charles Nzivo alisema kwamba ushirikiano huo utaafikiwa kupitia ubadilishanaji wa majarida, mipango ya utamaduni na kuvumisha lugha kati ya ubalozi na Maktaba tofauti nchini Kenya.

Akizungumza wakati wa mkutano na maafisa wa ubalozi wa China na usimamizi wa KNLS waliomtembelea katika ofisi yake kufuatilia mazungumzo ya awali kuhusu ushirikiano kati ya Embassy na KNLS, Dkt Nzivo alisema kwamba pande zote zilitambua ushirikiano uliopo ambao umeleta michango ya vitabu na ufadhili wa masomo wa mfanyakazi mmoja wa Maktaba ambaye alisafiri China kwa masomo ya uzamili kabla ya mkurupuko wa janga la Covid 19 mwaka wa 2020.

Afisa Mkuu Mtendaji huyo aliongeza kuwa timu hiyo ilijadili maeneo yaliyopendekezwa ya ushirikiano na kukubaliana kuangazia michango ya vitabu kufaidi Maktaba na vitabu kuhusu China katika matawi yote ya KNLS nchini Kenya.

"KNLS na ubalozi wa China zitashirikiana kuandaa tamasha za pamoja za filamu na maonyesho ya utamaduni katika Maktaba Kuu Nairobi, Nairobi, makao makuu yab KNLS na maktaba kubwa zaidi," alifichua Dkt Nzivo.

JANUAR1 17, 2023

# MyGov.

NAIROBI-KENYA I Issue No. 27/2022-2023

A PUBLICATION OF
**Government Advertising Agency**
Telposta Towers, Kenyatta Ave/ Koinange Street
P.O Box 30025-00100,
Nairobi Kenya
Telephone: (+254) 4920000 / 1
E-Mail: info@information.go.ke

## Egerton yakuza aina ya mimea inayotoa mavuno kukabili mabadiliko ya tabia nchi

**NA JANE NGUGI (KNA)**

Chuo Kikuu cha Egerton kwa ushirikiano na wadau wa kibinafsi na umma kimevumbua aina ya mimea inayotoa mavuno mengi na inayostahimili ukame na maradhi huku kikiendeleza juhudi za kuwafunza wakulima wakumbatie mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Miongoni mwa aina zinazotoa mavuno mengi na kustahimili ukame zilizoruhusiwa sokoni na taasisi hiyo ni pamoja na Egerton Mbaazi M1, Mbaazi M2 Mbaazi 3 na Mbaazi M4), aina mpya 29 za mhongo , aina mpya za maharagwe za Tasha, Ciankui na Chelalang ambazo zinastahili kwa maeneo yenye joto na mbegu za njugu aina ya Nyota na Mwangaza.

Zingine ni aina mpya za mtama za EUS 130, EUS1, EU-SS-10 na 'EU-SS-11 na mbaazi (Saina kal).

Mkurugenzi wa Bustani ya Kilimo -Sayansi wa Chuo Kikuu cha Egerton Profesa Paul Kimurto alisema kwamba kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, wadudu na maradhi ambayo hayakuwa au yaliyokuwa nadra yanaongezeka na kuathiri mavuno na kusababishia wakulima hasara. Profes



Kimurto alisema kwamba kutokana na hali ya mabadiliko ya tabia nchi inayoshuhudiwa, Chuo Kikuu hicho na washirika wake, kimejitahidi kufanya utafiti na kupata aina zinazoweza kuzoea athari za hali ya anga.

"Mabadiliko ya Tabia nchi yamekuwa tisho kwa utoshelevu wa chakula kote ulimwenguni. Athari zake zinajumuisha mvua isiyotabirika, na kupelekea mavuno kupungua na kuongezeka kwa gharama ya uzalishaji. Tukikosa kusaidia wakulima wetu kukumbatia kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabia nchi, uzalishaji utaendelea kupungua, na kusababisha mapato kupungua, watu kukosa kazi na njaa," alieleza.

Kwa kufanya utafiti na kukuza mbegu zinazostahimili mabadiliko ya tabia nchi, Chuo Kikuu cha Egerton kimekuwa kikishirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mimea kwa Maeneo Kame ya Kitropiki (ICRISAT), Shirika la Kukagua Ubora wa Mimea (Kephis), Mradi wa Utafiti wa Jamii (CARP+) na Shirika la Utafiti wa Kilimo na Ufugaji Kenya (KALRO).

Mashirika mengine ni Kituo cha Usimamizi wa Ubora katika Kilimo na Kilimobiashara Endelevu (CESAAM), kampuni ya East African Breweries Limited (EABL), Shirika la Ukanda la Kujenga Uwezo wa Vituo Vikuu katika Kilimo (RUFORUM), na Wakfu wa MasterCard na Alliance for a Green Revolution in Africa (Agra).

"Kunapaswa kuwa na ubunifu endelevu katika aina za mbegu zinazo stahimili ukame, aina zinatunza mazingira na usimamizi bora wa baada ya mavuno ili kupunguza hasara. Pia tumekuwa tukiwezesha wakulima waweze kufanya maamuzi yanayofaa kama kupanda wakati unaofaa na mumea unaostahili," alisema Profesa Kimurto. Kulingana na mhadhiri huyo, matumizi ya ubunifu na tekinolojia za kilimo kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ni kwa wakulima wa mashamba makubwa pekee.

"Ni muhimu kuwafunza wakulima wa mashamba madogo," anaongeza.

## Wanawake katika uchimbaji madini wajifunza ujuzi wa ufugaji wa nyuki

**NA ARNOLD LINGA MASILA (KNA)**

Kikundi cha kwanza cha wanawake 15 kutoka sekta ya uchimbaji mdogo wa madini katika kaunti ya Taita Taveta wameamua kupata mafunzo ya mwezi mmoja kuhusu mbinu bora za ufugaji wa nyuki ili wawe na ujuzi tofauti na kuwa na njia mpya bora za kujipatia mapato. Mafunzo hayo kwa usaidizi wa serikali ya kaunti na Catalyste+ yatawezesha wanawake hao kupata ufahamu na mafunzo halisi kuhusu jinsi ya kutumia ufugaji wa nyuki kama shughuli ya uchumi, sio tu kwa kupata asali lakini pia kwa kutoa bidhaa zingine, lakini pia mlango wa utalii biashara. Akizungumza akiwa Mwatate wakati wa kuanzisha mafunzo hayo, Waziri wa Biashara, Utalii na Ushirika wa kaunti hiyo Bi Gloria Monikombo, alisema kwamba mpango huo unatumia mbinu tofauti kwa kuwa utaunda nafasi za moja kwa moja za ajira kwa wanawake hao na pia kufungua nafasi kubwa zaidi kwa nafasi katika sekta ya utalii biashara eneo hilo.

"Tunautazama mpango huu kutoka pande tofauti. Kwanza, utaunda nafasi za ajira moja kwa moja kwa wanawake hao. Pili, utaunda mamia ya kazi kwa wakazi wanaotamani biashara utalii,"alisema Monikombo.

"Hawa ni wanawake wanaotegemea mapato yao madogo wanayopata kutoka uchimbaji madini mdogo na wakiongeza kitu zaidi katika ujuzi wao kutawawezesha kijamii na kiuchumi," aliongeza Monikombo. Wanawake katika uchimbaji mdogo wa madini wanachukuliwa kama kundi lililo kwenye hatari kwa kuwa wanahudumu katika hali ngumu ya kufanya kazi, malipo duni na wakati mwingine wanadhulumiwa kingono na wenzao wanaume. Mafunzo kuhusu ufugaji nyuki kulingana na

Livingstone Mghenyi, Mwenyekiti wa Kitaifa wa Chama cha Utalii wa Ndani (DTA), ni shughuli ya kujikimu kimaisha ya wanawake kujiunga na shughuli ya kiuchumi isiyo hatari na yenye faida huku wakati huo huo ikipanua sekta ya biashara ya utalii katika kaunti hiyo.

Mghenyi aliongeza kuwa mafunzo hayo ni mwanzo wa mipango ya muda mrefu ya kaunti hiyo kuwa mdau mkubwa katika sekta ya ufugaji nyuki na kuongeza sekta nyingine ya kuvutia watalii kwa kapu ya vivutio kama wanyama pori na madhari asili katika kaunti hiyo. "Tunaanza mpango wa muda mrefu wa kubadilisha kaunti hii kuwa kiongozi katika sekta ya ufugaji nyuki na pia kuongeza vivutio vya utalii," alisema Mghenyi.

## KWA UFUPI

### Huduma za picha za CT zaanzisha Homa Bay

Wakazi wa Homa Bay sasa wataweza kutambuliwa magonjwa wanayougua haraka, baada ya mtambo wa Computerized Tomography (CT) Scan wa gharama ya Sh40 milioni na kituo cha wagonjwa wa kutibiwa na kurudi nyumbani kuanzishwa katika hospitali ya Mafunzo na Rufaa ya Kaunti.

Akianzisha miradi hiyo, Gavana Gladys Wanga, alisema vifaa vya picha ya CT scan vitaimarisha kasi na usahihi wa utambuzi wa magonjwa, kuhakikisha wagonjwa wanapatiwa huduma bora za afya inavyowezekana.

Wanga alisema ni ufanisi mkubwa kwa serikali yake kutimiza ndoto yake ndani ya siku 100 ofisini alivyoahidi wakazi wakati wa kampeni.

"Serikali yangu itaendelea kuwekeza katika na kuimarisha mfumo wa afya ili kila mkazi aweze kuwa na maisha bora inavyowezekana," alisema.

Gavana huyo alisema kwamba kaunti inapanga kujenga jengo la ghorofa kadhaa ya vitengo vya ajali na dharura kabla ya mwisho wa mwaka. "Tunatarajia kwamba kufikia mwisho wa mwaka, kwa mapenzi ya Mungu, tutarudi mahali hapa kufungua rasmi kituo cha ajali na dharura na kitengo kipya cha wagonjwa wa kutibiwa na kurudi nyumbani," alisema gavana huyo. Aliongeza kuwa vitengo vipya vilivyojengwa ni mwanzo tu wa hatua kubwa za maendeleo katika sekta ya afya. Mkuu huyo wa kaunti alisema kwamba Hazina ya Taifa ya Bima ya Afya (NHIF) italipia huduma za CT Scan na akahimiza wakazi kujisajili na kutumia kituo hicho. Wanga alisema kwamba kuimarishwa kwa kitengo cha kusafisha damu kunaendelea na akasema imekuwa changamoto kwa muda mrefu licha ya idadi ya wagonjwa wanaohitaji huduma hizo kuongezeka. Kituo hicho kipya kiko na chumba cha kisasa cha upasuaji kinachoweza kutumiwa kufanya upasuaji 8-10 kwa siku.

Alisema kwamba, awali, wagonjwa kutoka kaunti ya Homa Bay wamekuwa wakitumwa Kisumu kwa huduma za CT scan. "Kuanzia leo, wagonjwa hawatakuwa wakitumwa tena, ni wagonjwa kutoka kaunti jirani kama Migori ambao watakuwa wakitumwa katika kituo chetu," alisema.Alisema CT scan pia itakuwa chanzo cha mapato kwa sekta ya afya lakini akasisitiza utoaji wa huduma kwa wakazi wa kaunti ya Homa Bay ni muhimu zaidi.

### Serikali kuimarisha mpango wa kutoa pesa wa Inua Jamii

Mpango wa serikali wa kutumia pesa wasiojiweza wa Inua Jamii utanyooshwa ili kuimarisha utendaji, uwajibikaji na kufaidi watu wengi, Katibu wa Kinga ya Jamii Joseph Motari amesema.

Motari alisema hii ni kulingana na ahadi ya manifesto ya Kenya Kwanza kuimarisha maisha ya watu wazee na watu wanaoishi na ulemavu.

Akizungumza akiwa Kajiado wakati alipofuatilia ulipaji wa malipo ya Julai-Agosti 2022 na Septemba-Oktoba 2022 kwa wanaonufaika na Inua Jamii Motari alihakikishia wanaonufaika kwamba malipo yatakuwa yakitolewa kwa wakati akisema ya mikumbo miwili yalicheleweshwa kufuatia mpito kutoka serikali iliyoondoka hadi serikali ya Kenya Kwanza.

" Tunataka kuhakikishia wanaonufaika na mpango wa Inua Jamii kwamba serikali itatoa pesa zao kwa wakati ili kuwakinga walio katika hatari na wazee katika jamii dhidi ya umasikini," alisema Motari. Hata hivyo, Katibu huyo alihimiza wanaonufaika kote nchini kutumia pesa zao vyema ili waishi maisha bora.

Motari alisema kwamba kama sehemu ya kuimarisha utendaji, benki sita ambazo zimepatiwa kandarasi ya kutoa malipo hayo zimeruhusiwa kuwa na maajenti katika wadi na kaunti ndogo kote nchini kutoa pesa hizo Kwa wanaonufaika. Alisema hii itaokoa wazee wanaotembea mwendo mrefu na kuwaepushia gharama na uchovu na matatizo mengine.

Katibu alihimiza wanaotimiza mahitaji ya mpango huo kujisajili na maafisa wanaohusika katika kaunti ndogo akisema usajili unafanyika kila wakati.

Motari alisema kwamba serikali inataka kuanzisha sajili moja kuepuka mtu mmoja kunufaika mara mbili.

Alisema kwamba serikali kwa ushirikiano na Benki ya Dunia itasajili wote wanaonufaika na Hazina ya Taifa ya Bima ya Afya (NHIF) kutimiza ahadi ya Kenya Kwanza ya kuweka wazee wote katika NHIF ndani ya miaka mitatu.

Wiki jana, serikali ilitoa Sh8.58 bilioni kwa watu 1.07 milioni wanaonufaika na mpango huo kote nchini.

*Na Odhiambo Omondi (PCO)*

REPUBLIC OF KENYA

GAA GOVERNMENT ADVERTISING AGENCY

KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD

**DESIGN AND EDITING OF MYGOV WEEKLY BY THE KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD**
NHIF Building , 4th Floor, P.O. Box 34035-00100
Tel: 0202715390 / 0757029456
Email: info@kenyayearbook.go.ke
www.kenyayearbook.co.ke